MCHAKATO WA KUPANGA KIMKAKATI

Dakika 40

(Wagawe washiriki katika vikundi kulingana na makanisa yao au katika vikundi vya watu wanne hadi watano. Wape kila kikundi kipande kikubwa cha karatasi. Elezea kwamba wataunda picha ya huduma ya kanisa lao kwa familia, sasa na kwa siku zijazo – sawa na shughuli katika somo la 6.

Toa mfano/maagizo kwenye ubao. Acha washiriki wachore njia kutoka upande mmoja wa karatasi yao hadi nyingine, ikiwakilisha njia ya ukuaji wa kanisa katika huduma kwa familia. Kisha soma na ueleze maswali, ukitoa dakika tano kwa kila swali kwa vikundi kuchora na kuandika majibu yao.)

1. **Tuko wapi sasa?** Kwanza, kwenye upande wa kushoto wa chini wa ukurasa, chora au elezea kwa maneno huduma ya sasa ya kanisa lako kwa familia. Alama au mchoro wa vijiti ni sawa. Fikiria unachofanya, wapi wanakutana, ni familia ngapi zinazohudhuria hafla, rasilimali zipi zinapatikana, ni nani anayehusika kuhudumia, nk.
2. **Tunataka kuwa wapi?** Kisha, katika upande wa juu wa kulia wa ukurasa, chora au elezea huduma bora ya kanisa lako kwa familia. Fikiri kupitia mafunzo yanayofundishwa katika mafunzo haya ili kuongoza fikra zako. Je, ni maono gani ya kanisa lako kwa huduma ya familia kwa miaka mitano ijayo, miaka 25 ijayo? Familia zenye afya zingeonekanaje? Je, kanisa lingekuwa likifanya nini kutegemeza na kuendeleza nyumba zenye nguvu, zinazomzingatia Kristo? Ni nini athari inayotarajiwa kwa jamii?
3. **Tunafikaje huko?** Chora njia kati ya pande za chini kushoto na juu kulia za karatasi. Linganisha sehemu mbili zilizotangulia, “Tulipo,” na “Mahali tunapotaka kuwa,” na uje na hatua fulani za vitendo jinsi sisi, kwa uwezo wetu, rasilimali, na imani, tunaweza kufanya ndoto hii kuwa kweli. Je, kuna mambo tunayohitaji kuanza au kuacha kufanya? Je, tunaweza kufanya nini ili kuwawezesha na kuwategemeza wazazi ili kuwasaidia kuwa wafanya-wanafunzi wazuri? Ikiwa kanisa haliwezi kukidhi kila hitaji la familia, kanisa letu linaweza kutimiza mahitaji gani? Andika baadhi ya maneno au mawazo muhimu kwenye njia kati ya sasa na yajayo, ukikumbuka kuwa ni sawa kuanza polepole unapoanzisha mabadiliko.
4. **Nani atasaidia safari hii?** Je, kuna watu wengine, matukio, huduma au vikundi ambavyo vinaweza kusaidia maono yetu kuwa ukweli? Je, tunashiriki maono na nani ili kuwasaidia wengine kuwaona wazazi kama washirika katika huduma? Huduma ya watoto na wafanyakazi wa watoto wanawezaje kuwatiamoyo na kuwa utegemezo kwa familia wanapowafunza watoto wao? Ni kwa jinsi gani kanisa zima linaweza kutoa faraja na usaidizi kwa familia wanapowafunza watoto wao? Chora na uweke lebo kwenye matukio hayo, vikundi na watu kwenye nafasi wazi juu ya njia.
5. **Ni nani au ni nini kinachoweza kuzuia safari hii?** Ni kwa njia gani adui angeharibu maono haya? Je, tunaweza kukabiliana na vikwazo au changamoto gani? Je, tunajitayarishaje kwa changamoto zinazokuja? Chora na uweke lebo kwenye changamoto hizo katika nafasi wazi chini ya njia.

(Toa jumla ya dakika 25 kwa vikundi kujadili na kuchora. Kisha waambie washiriki picha zao na kikundi kingine kimoja. Ikiwa ni wakati, vikundi vyote vishiriki picha zao na kikundi kizima.)

Tuna mawazo/mambo mengi mazuri ya kufikia/kufunza familia katika makanisa yetu. Lakini ni lazima tutafute mwongozo wa Mungu na kumfuata kwa utii. Hebu tuweke mipango hii kwake. (Funga kwa wakati wa maombi.)